NCDC
NATIONAL CURRICULUM DEVELOPMENT CENTRE

# SILABASI YA KISWAHILI

## DARASA LA NNE

2022

NATIONAL CURRICULUM DEVELOPMENT CENTRE

# SILABASI YA KISWAHILI

## DARASA LA NNE

2022

A product of the National Curriculum Development Centre for the Ministry of Education and Sports with support from the Government of Uganda 2022

**National Curriculum Development Centre**
P.O. Box 7002,
Kampala- Uganda
www.ncdc.go.ug

**ISBN: 978-9970-675-56-2**

All rights reserved: No part of this publication may be reproduced, stored in a retrieval system or transmitted in any form or by any means, electronic, mechanical, photocopying, recording, or otherwise, without the prior permission of the copyright holder.

# CONTENTS

**DIBAJI (PREFACE) ....... IV**
**FOREWORD ....... V**
**ACKNOWLEDGEMENTS....... VI**
**USULI WA MTAALA WA KISWAHILI NCHINI UGANDA ....... 1**
MALENGO YA ELIMU YA TAIFA....... 1
MALENGO YA ELIMU YA MSINGI NCHINI UGANDA....... 2
**MPANGILIO WA SILABASI YA LUGHA YA KISWAHILI ....... 3**
**UMUHIMU WA KUFUNDISHA LUGHA YA KISWAHILI ....... 3**
**MBINU ZA KUFUNDISHIA ....... 4**
**VIFAA VYA KUFUNDISHIA....... 4**
HATUA ZA UFUNDISHAJI ....... 4
**HATUA YA I: UKUZAJI WA STADI ZA KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ....... 5**
KUSIMULIA HADITHI ....... 5
MASHAIRI....... 5
MAZUNGUMZO ....... 5
PICHA....... 6
HATUA YA II: KUFUNDISHA MSAMIATI ....... 6
HATUA YA III: KUFUNDISHA STADI YA KUSOMA....... 6
HATUA YA IV: KUFUNDISHA VIPENGELE VYA KISARUFI ....... 6
KUFUNDISHA KWA KUPITIA DIALOJIA....... 7
KUFUNDISHA KWA KUPITIA MICHEZO ....... 7
KUFUNDISHA KWA KUPITIA DRAMA ....... 7
HATUA YA V: KUFUNDISHA STADI YA KUANDIKA ....... 7
**TATHMINI ....... 8**
VIPINDI PENDEKEZWA KWA KILA SOMO....... 8
SAMPULI YA RATIBA PENDEKEZWA KWA DARASA LA NNE ....... 9
**MUHULA WA KWANZA ....... 10**
MADA KUU 1: ALFABETI, SALAMU NA ADABU ....... 10
MADA KUU 2: UKOO ....... 13
MADA KUU 3: MWILI WA BINADAMU ....... 17
MADA KUU 4: HESABU ....... 21
**MUHULA WA PILI ....... 24**
MADA KUU 1: MAVAZI NA RANGI....... 24
MADA KUU 2: WANYAMA ....... 27
MADA KUU 3: AFYA NA USAFI ....... 30
**MADA KUU 4: SEHEMU ZA NYUMBANI....... 33**
**MUHULA WA TATU ....... 36**
MADA KUU1: MICHEZO ....... 36
**MADA KUU 2: BIASHARA ....... 39**
**MADA KUU 3: UONGOZI ....... 41**

# DIBAJI (PREFACE)

Lengo kuu la silabasi ya Kiswahili ya darasa la nne litatekelezwa iwapo walimu watazingatia mambo yote muhimu husika ipasavyo. Mwalimu anatarajiwa kuwa mbunifu zaidi ili kutekeleza yafuatayo;

Kufasiri na kutumia silabasi kwa namna inayostahili.

Kuandaa mazingira ya kufundishia ambayo yatamshirikisha mwanafunzi kikamilifu katika mchakato wa ujifunzaji.

Kutumia vifaa bora vya kufundishia kwa kusisitiza lengo na hali halisi katika mazingira ya ndani na nje ya shule.

Kushirikisha raslimali watu watakaopatikana ndani na nje ya shule.

Kutumia mbinu na mikakati maalumu katika tathmini kwa wakati unaofaa.

Mwalimu anashauriwa kujiendeleza kiutafiti ili aweze kuimarika katika matumizi ya msamiati na istilahi za lugha ya Kiswahili ili kuwasiliana kiufasaha.

Silabasi hii imeasisiwa ili kumpa mwalimu mbinu za kimsingi za kufundishia Lugha ya Kiswahili. Walimu pia wanashauriwa kuzingatia na kufuatia mapendekezo yaliyotolewa katika silabasi hii na hata kuboresha popote patakapokuwa na mahitaji.

## FOREWORD

The Syllabus is a key curricular material which must be available to every teacher of a subject. It offers vital suggestions to the teacher on what to teach and how he/she can manage a teaching and learning situation of a given subject. Then the teacher depending on his/her professional preparedness and experience can adjust, modify or reflect the suggestions from an informed point of view.

The Syllabus and Teachers' Guide for Kiswahili language have been designed in a unique way to address the nature of the subject. Teachers should not only use it but also make constructive inputs for its improvement.

The Constitution of Uganda prescribes Kiswahili as a Second Official Language to be used in such circumstances as Parliament may by law prescribe. Further, Uganda as one of the East African Community member states is tasked to spear head the spread and use of Kiswahili language unto its citizens. To achieve this, Kiswahili was introduced in the education system.

To this effect, National Curriculum Development Centre through the Ministry of Education and Sports developed Kiswahili curriculum for primary schools as a timely response to the national needs.

I therefore, urge all stakeholders involved in Kiswahili curriculum implementation to give it full support from all points of view to ensure its success.

**Prof. George Ladaah Openjuru**
Chairperson, NCDC-Governing Council

## ACKNOWLEDGEMENTS

The National Curriculum Development Centre (NCDC) would like to express its appreciation to all those who worked tirelessly towards the production of this Kiswahili syllabus.

Our gratitude goes to the Ministry of Education and Sports for overseeing and taking timely decisions whenever necessary. Our thanks also go to partners in education who provided the professional information and technical assistance and guidance to enable us come up with this Syllabus of Kiswahili.

We also extend our gratitude to members of the Kiswahili subject panel and all those who worked behind the scenes, tirelessly and deligently supporting the team to finalise this syllabus and ensure its timely production.

The National Curriculum Development Centre takes responsibility for any shortcomings that might be identified in this publication and welcomes suggestions for effectively addressing the inadequacies. Such comments and suggestions may be communicated to NCDC through our contact addresses; P.O Box 7002, Kampala or Email: *admin@ncdc.go.ug or www.ncdc.go.ug*

**DR. GRACE K. BAGUMA**
Director,
National Curriculum Development Centre

## USULI WA MTAALA WA KISWAHILI NCHINI UGANDA

Ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda ulianza miaka ya utawala wa kikoloni. Baadaye, lugha hii ilipata upinzani kutoka mashirika mbalimbali kama wamishonari, watawala wa kitamaduni na baadhi ya wakoloni. Upinzani huu ulisababisha lugha hii kuondolewa katika mfumo wa elimu.

Mwaka 1972, serikali ya Rais Idi Amini Dada ilipendekeza Kiswahili kuwa lugha ya taifa. Hata hivyo, pendekezo hilo halikutekelezwa. Serikali ya NRM ilipochukua madaraka mwaka 1986 ilidhihirisha mtazamo chanya kuhusu Kiswahili. Mwaka 1987 tume iliyoongozwa na Profesa Ssenteza Kajubi iliundwa kwa lengo la kupitia upya sera ya elimu nchini Uganda. Tume hii ilipendekeza kuwa lugha ya Kiswahili ifundishwe katika shule zote nchini Uganda. Aidha, hati ya serikali ya kutekeleza mapendekezo hayo ya mwaka 1992 ilisisitiza ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili katika shule za msingi.

Kutokana na msingi wa mapendekezo hayo, Wizara ya Elimu na Michezo kupitia Kituo cha Taifa cha Ukuzaji wa Mitaala, imeandaa mtaala wa kutumika katika mchakato wa kufundisha Kiswahili katika shule za msingi.

### MALENGO YA ELIMU YA TAIFA

Mtalaa huu umetayarishwa ili kutekeleza malengo ya taifa ya elimu kama yanavyotajwa katika hati ya serikali juu ya ripoti ya uboreshaji wa Sera ya Elimu ya mwaka 1992. Malengo haya ni yafuatayo:

1. Kukuza utambuzi wa thamani ya umoja wa kitaifa, uzalendo pamoja na utamaduni kwa kuzingatia uhusiano wa ndani pamoja na umuhimu wa kutegemeana.
2. Kuwawezesha wanafunzi kuwa na maadili ya kiroho na utu wema, pamoja na kukuza nidhamu, uungwana, uvumilivu na uhusiano mwema.
3. Kuwatia Wanauganda moyo wa kuhudumia wengine, kupenda kazi na uongozi ili kushiriki katika mambo ya uananchi, ya jamii na ya kitaifa kupitia shughuli za pamoja katika asasi za elimu na jamii.
4. Kukuza maarifa ya kisayansi, kiufundi na kitamaduni, stadi na mitazamo inayohitajika kustawisha maendeleo ya nafsi na taifa kwa ujumla.

5. Kumpa mtu binafsi stadi za msingi na maarifa ya kutumia katika mazingira yake ili kujiendeleza na kuliendeleza taifa; kwa afya nzuri, lishe bora na maisha ya familia pamoja na uwezo wa kujiendeleza kielimu.
6. Kuwapa wanafunzi uwezo wa kuchangia ujenzi wa uchumi wa taifa, wa kujitegemea na kudumu katika hali mbalimbali.

## MALENGO YA ELIMU YA MSINGI NCHINI UGANDA

Katika kiwango cha elimu ya msingi, malengo ya taifa yanaweza kuwasilishwa kwa kujumuisha malengo na shabaha zifuatazo;

1. Kuwawezesha watu binafsi kupata umilisi wa kusoma, kuandika, kuhesabu na stadi za kuwasiliana nchini.
2. Kuwaendeleza na kuwaimarisha wanafunzi kiafya na kiakili.
3. Kuwawezesha wanafunzi kuwa na maadili mema kwa kushirikiana na kujali watu wengine katika jamii.
4. Kuendeleza utamaduni, maadili na dini katika maisha ya wanafunzi.
5. Kuwawezesha wanafunzi kuthamini na kulinda mazingira wakitumia maarifa ya sayansi na ya teknolojia.
6. Kuendeleza uzalendo, umoja, utambuzi wa haki, wajibu wa kila mtu na utambuzi wa haja ya ushirikiano nchini.
7. Kuendeleza hali ya kudumisha elimu na maendeleo.
8. Kukuza stadi za utendaji za kujikimu maishani.
9. Kukuza upendaji wa kazi pamoja na moyo wa kujitegemea mwenyewe.
10. Kukuza uwezo wa kutumia mkabala wa kutafuta suluhisho katika hali mbalimbali za maisha.
11. Kuendeleza nidhamu na tabia nzuri miongoni mwa wanafunzi.

## MPANGILIO WA SILABASI YA LUGHA YA KISWAHILI

Silabasi ya Kiswahili ya darasa la nne imepangwa kwa njia ambayo inakuza ufasaha kwa mwanafunzi. Mpangilio huu umefanywa ili kumwezesha mwanafunzi kujifunza Kiswahili bila utata.

Kufanikisha haya yote, mada za msingi za ngazi ya darasa la nne zimeshughulikiwa. Vilevile, vipengele vya lugha ambavyo hukuza ufasaha wa lugha vimepangwa kutoka katika kiwango cha chini hadi kiwango cha juu kwa mchakato wa kumwezesha mwanafunzi kutambua na kukuza lugha ya Kiswahili.

Mpangilio huu utamsaidia mwanafunzi ambaye anajifunza lugha hii kwa mara ya kwanza kupata ufasaha kwa haraka.

Kila mada kuu ina vipengele kati ya saba na tisa. Muhula wa kwanza una mada kuu nne, muhula wa pili una mada kuu nne pia muhula wa tatu una mada kuu tatu.

Mpangilio huu umezingatia stadi nne za lugha pamoja na stadi za kudumu na utamsaidia mwanafunzi kukuza msamiati wake pamoja na kuutumia katika mazungumzo kwa sababu lugha hii ni nyepesi na inaendana na kiwango cha mwanafunzi.

## UMUHIMU WA KUFUNDISHA LUGHA YA KISWAHILI

Lugha ya Kiswahili inafaa kufundishwa katika shule za Uganda kwa sababu ya umuhimu wake; yaani ni lugha ambayo:

- Ina uwezo wa kuwaunganisha Wanauganda wote kwa sababu haimilikiwi na kabila lolote.
- Itarahisisha mawasiliano miongoni mwa watu wa eneo la Afrika Mashariki.
- Hii ni lugha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- Itawawezesha watu kufanya biashara hata nje ya Uganda bila vikwazo.
- Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Muungano wa nchi za Afrika. (AU)
- Inatambuliwa miongoni mwa lugha muhimu saba za Dunia na shirikisho la kimataifa (UNO).
- Inatumiwa Kimataifa kwenye vituo mbalimbali vya redio na runinga duniani kama vile VOA, BBC, DW na CCTV.

- Inafundishwa katika vyuo vikuu mbalimbali vya Afrika Mashariki na hata vya nje ya Afrika kama vya Marekani na kwingineko.
- Imesaidia watu kuajiriwa katika mashirika anuwai.
- Imeingizwa katika mtandao wa intaneti.

## MBINU ZA KUFUNDISHIA

Mbinu ambazo zimependekezwa kufundishia Kiswahili ni zile ambazo zinahusisha wanafunzi wote pamoja na wale wenye mahitaji maalumu. Aidha, matumizi ya vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yanahimizwa. Mwalimu anashauriwa kuhimiza shughuli zinazoendeleza stadi za utafiti miongoni mwa wanafunzi wake.

Zifuatazo ni baadhi ya mbinu ambazo mwalimu anaweza kutumia katika shughuli za mafunzo mbalimbali: majadiliano, makundi, udhihirishaji, utafiti, matembezi, uwasilishaji, uigizaji, nyimbo, ukariri, uchoraji, ufinyanzi, n.k. Hata hivyo, anaweza kupendekeza mbinu nyingine mwafaka au kuchagua ile inayofaa kutegemea mahitaji ya funzo.

## VIFAA VYA KUFUNDISHIA

Matumizi ya vifaa bora vya kufundishia huchangia sana katika ufundishaji na kuelewa kwa mwanafunzi.
Kwa hivyo, mwalimu wa Kiswahili anashauriwa kutengeneza na kutumia vifaa vya aina mbalimbali katika ufundishaji.
Mwalimu anaweza kujitengenezea vifaa vyake mwenyewe kama vile kadi za maneno, mistari, chati, michoro, vifaa vya kiteknolojia, nk.
Vifaa vya kufundishia ni lazima viwe vinaambatana na mada ambayo inalengwa kufundishwa.

### Hatua za ufundishaji

Hatua za ufundishaji zimeshughulikiwa katika mwongozo wa mwalimu zikizingatia stadi zote nne za lugha na stadi za kudumu.

Katika hatua hizi, ufundishaji wa masimulizi, ushairi, msamiati, methali, semi, vitendawili, vipengele vya kisarufi, kusoma na kuandika vimeshughulikiwa kikamilifu. Mwalimu anashauriwa kufuata hatua hizo na vilevile kufanya mabadiliko ya hatua hizi kutegemea viwango vya umilisi wake na wanafunzi.

## HATUA YA I: Ukuzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu anashauriwa kufundisha stadi hizi kwa kuzingatia yafuatayo;

**Kusimulia hadithi**

i) Kusoma hadithi
ii) Kusimulia hadithi
iii) Kuwashirikisha wanafunzi kusimulia hadithi
iv) Kuwaongoza kujadiliana kuhusu hadithi
v) Kuwauliza maswali ya kimapokezi kuhusu hadithi
vi) Kubainisha ujumbe katika hadithi
vii) Kutaja mafunzo yatokanayo na hadithi

**Mashairi**

i) Kusoma shairi
ii) Kukariri shairi
iii) Kuigiza kwa kukariri shairi
iv) Kueleza ujumbe wa shairi
v) Kutaja ujumbe wa shairi
vi) Kuimba shairi
vii) Kutaja ujumbe na funzo katika shairi

**Mazungumzo**

i) Mwalimu kuwaongoza kusoma mazungumzo
ii) Kushirikisha darasa kusoma mazungumzo
iii) Kutumia makundi kusoma mazungumzo
iv) Kuchagua wanafunzi kuigiza mazungumzo kwa kusoma
v) Kuigiza mazungumzo darasani
vi) Kutaja ujumbe na mafunzo ya mazungumzo
vii) Kujibu maswali ya kimapokezi

## Picha

i) Kuwaongoza wanafunzi kufasiri picha
ii) Kueleza kuhusu picha
iii) Kusimulia vitendo katika picha
iv) Kutunga sentensi kuhusiana na picha

## Hatua ya II: Kufundisha msamiati

i) Kuwashirikisha wanafunzi kutambua msamiati waliousoma
ii) Kuorodhesha msamiati husika
iii) Kuelekeza wanafunzi kusoma msamiati
iv) Kushirikisha wanafunzi kueleza maana ya msamiati
v) Kutumia picha, michoro na vifaa halisi kuelezea kuhusu maana ya msamiati
vi) Kuongoza wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia msamiati
vii) Kushirikisha wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia msamiati
viii) Kuwapa wanafunzi zoezi la kutunga sentensi, kujaza mapengo, kuchora vitu nakadhalika

## Hatua ya III: Kufundisha stadi ya kusoma

i) Kushirikisha wanafunzi kusoma hadithi au taarifa
ii) Kuchagua mwanafunzi mmoja baada ya mwingine kusoma
iii) Kuongoza kutaja mambo muhimu
iv) Kuwashirikisha katika kujadili ujumbe wa makala
v) Kuwauliza maswali kuhusiana na makala
vi) Kuwapa zoezi la kubainisha ujumbe muhimu katika makala/ taarifa/ hadithi

## Hatua ya IV: Kufundisha vipengele vya kisarufi

i) Kupitia msamiati waliousoma
ii) Kutambua kipengele cha kisarufi
iii) Kuwashirikisha katika kueleza kuhusu kanuni za kisarufi za kipengele husika
iv) Kuwaongoza katika kueleza na kutaja vipengele husika
v) Kuwashirikisha katika kutunga sentensi kwa kuzingatia kanuni na kutumia msamiati waliojifunza.
vi) Kuongoza wanafunzi katika kueleza maana ya sentensi
vii) Kuwaelekeza kufanya zoezi la kisarufi
viii) Kupitia kazi ili kusisitiza kanuni ya kisarufi waliyojifunza.

## Kufundisha kwa kupitia dialojia

i) Kuwaongoza kupitia msamiati waliojifunza
ii) Kuhakikisha kuwa wanafunzi wanatambua maana ya msamiati au kipengele husika
iii) Kuwaongoza wanafunzi kurudia kutambua kipengele walichojifunza
iv) Kuwaweka wanafunzi katika vikundi viwili
v) Kuwaelekeza wanafunzi kufanya dialojia
vi) Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi kuigiza kuhusu dialojia husika
vii) Kuwaelekeza wanafunzi kudhihirisha uwezo wao wa dialojia mbele ya wanafunzi wenzao.

## Kufundisha kwa kupitia michezo

i) Kuwashirikisha wanafunzi kutambua maana ya msamiati unaopatikana katika mchezo
ii) Kutoa maelekezo ya jinsi mchezo huo unavyochezwa
iii) Kudhihirisha mchezo kwa kuigiza mbele ya wanafunzi
iv) Kuchagua wanafunzi walio na uwezo wa kushiriki katika kuigiza mchezo
v) Kuwaongoza wanafunzi kuigiza mchezo wenyewe.

## Kufundisha kwa kupitia drama

i) Kutumia hatua za kufundisha kupitia mchezo.
ii) Kuwaongoza wanafunzi katika uigizaji bila masharti.

## Hatua ya V: Kufundisha stadi ya kuandika

i) Kuandika maneno kwa tahajia sahihi
ii) Kukamilisha sentensi.
iii) Kuandika maneno katika mashindano, mwalimu anawaambia wanafunzi kuandika kwa kasi maneno anayowasomea ili aone ni nani atakayekuwa wa kwanza kumaliza. n.k

# TATHMINI

Tathmini ni sehemu muhimu katika ufundishaji kwa sababu inasaidia kupima uwezo na maendeleo ya mwanafunzi.

Katika silabasi hii, aina ya tathmini ambayo imependekezwa ni tathmini endelevu kwa mwanafunzi. Tathmini hii inatokana na mafunzo pendekezwa. Njia hii itamsaidia mwalimu wa Kiswahili kupima umilisi wa wanafunzi ili aweze kuwapa mafunzo bora zaidi.

Masomo ya ziada ambayo yatatayarishwa na mwalimu, yanatokana na upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi katika shughuli za darasani. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi darasani unamsaidia mwalimu kukuza stadi mbalimbali za mwanafunzi. Kwa hivyo, tathmini endelevu kwa mwanafunzi ni lazima iendane pamoja na mafunzo.

## VIPINDI PENDEKEZWA KWA KILA SOMO

Lugha ya Kiswahili itakuwa na vipindi vitatu kila wiki. Vipindi hivi vitatolewa kwa Kiingereza (kipindi kimoja kila darasa); Hisabati, (kipindi kimoja kila darasa) sanaa za kubuni; (kipindi kimoja toka darasa la nne) na kipindi kimoja kutoka wakati wa maktaba kwa darasa la 5 – 7. Mgawanyo huu unaoneshwa katika jedwali lifuatalo:

| SOMO | | VIPINDI | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | P.4 | P.5 | P.6 | P.7 |
| 1 | Kiingereza (English) | 6 | 6 | 6 | 6 |
| 2 | Mafunzo ya Elimujamii (Social Studies) | 5 | 5 | 5 | 5 |
| 3 | Dini (RE) | 3 | 3 | 3 | 3 |
| 4 | Hisabati (Maths) | 6 | 6 | 6 | 6 |
| 5 | Sayansi (Integrated Science) | 7 | 7 | 7 | 7 |
| 6 | Lugha Mama(Local Language) | 3 | 3 | 3 | 3 |
| 7 | Kiswahili | 3 | 3 | 3 | 3 |

| **SOMO** | | **VIPINDI** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | Sanaa za Kubuni na Elimu ya Haiba na Michezo (Creative Arts and PE) | 6 | 6 | 6 | 6 |
| 9 | Maktaba (Library) | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | Jumla (Total Periods) | 40 | 40 | 40 | 40 |

## Sampuli ya Ratiba pendekezwa kwa Darasa la Nne

| Day | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Eng | Mth | CAPE | | SCE | SCE | SST | | RE | Lib | |
| Tue | mth | Eng | Kisw | ***BREAK*** | SST | Mth | CAPE | ***LUNCH*** | SCE | | ***GAMES*** |
| Wed | SCE | SST | CAPE | | Mat | Eng. | ENG | ***BREAK*** | Eng | LL | |
| Thur | RE | Eng | SCE | | SST | Mth | SCE | | Kisw | CAPE | |
| Friday | Mth | Kisw | CAPE | | Eng. | RE | LL | | CAPE | SST | |

**Key**

**CAPE:** *Creative Arts and Physical Education*
**SCE:** *Integrated Science with Agriculture*
**RE:** *Religious Education*
**Lib:** *Library*
**SST:** *Social Studies*
Mth: *Mathematics*
Kisw: *Kiswahili*
LL: *Local Language*

# MUHULA WA KWANZA

## MADA KUU 1: ALFABETI, SALAMU NA ADABU

**Usuli:** Mafunzo haya yatamwezesha mwanafunzi kubainisha sauti za Kiswahili na msamiati unaohusiana na adabu ili aweze kuwasiliana katika shughuli za kila siku.

**Matarajio:**

- Mwanafunzi aweze kutamka sauti za Kiswahili kwa usahihi.
- Mwanafunzi awasiliane kwa kutumia salamu, maneno ya adabu na vipengele vya kisarufi.

**Stadi za kimaisha na maadili**

Kuwasiliana kwa ufasaha:

i) Kuheshimu kupitia:
  - Maneno ya adabu
  - Salamu

ii) Upendo kwa sababu ya kuonesha heshima na kunyenyekea

iii) Kuthamini kwa kuwasiliana na kujuliana hali

iv) Kutambua na kujitambua

v) Kushirikiana kwa kuonyesha upendo na kujuliana hali.

| Umilisi | Yaliyomo | Shughuli zinazopendekezwa |
|---|---|---|
| **Mwanafunzi:**<br>• Atamke vokali na konsonanti kwa usahihi<br>• Aunganishe vokali na konsonanti kuunda silabi<br>• Aunde maneno kutoka kwa silabi | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>a) Alfabeti ya Kiswahili<br>(i) A, e, i, o, u<br>(ii) B, ch, d, f, g, gh, h, j, k......... | • Kusikiliza na kutambua matamshi ya sauti za Kiswahili.<br>• Kutamka sauti za Kiswahili kwa usahihi.<br>• Kuunda maneno kutoka kwa silabi |

| Umilisi | Yaliyomo | Shughuli zinazopendekezwa |
|---|---|---|
| • Atamke sauti za alfabeti ya Kiswahili kwa usahihi | | |
| • Asalimie na kujibu salamu<br>• Atamke maneno ya adabu ipasavyo | b) Salamu<br>Salamu za wakati na hali<br>• Habari ya:<br>- asubuhi?<br>- mchana?<br>- adhuhuri?<br>- jioni?<br>• U hali gani?<br>• Umelala je? | • Kuigiza salamu za wakati na hali<br>• Kuambatanisha salamu na jibu |
| • Atumie msamiati unaohusiana na salamu katika sentensi | Ch) Msamiati<br>Maneno ya adabu k.v.:<br>- pole<br>pole kwa msiba<br>- shukrani<br>- nisamehe<br>- naomba msamaha<br>- nakushukuru<br>- tunakushukuru<br>- lala salama<br>- usiku mwema | • Kutaja msamiati wa adabu<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia msamiati wa adabu<br>• Kudhihirisha adabu katika mazungumzo<br>• Kuigiza kuhusu adabu |
| Asome na kuigiza mazungumzo kwa sauti na kwa ufasaha | **Kusoma**<br>Mazungumzo yanayodhihirisha maamkuzi na matumizi ya maneno ya adabu k.v.:<br>**Masaba**: Hodi? | • Kusoma mazungumzo yanayodhihirisha adabu<br>• Kurekodi maigizo ya salamu na maneno ya adabu kwa kutumia |

| Umilisi | Yaliyomo | Shughuli zinazopendekezwa |
|---|---|---|
| | **Nantume**: Karibu. | kamera, simu, kompyuta nk. |
| • Atambue nomino katika ngeli ya a-wa<br>• Atamke nomino katika ngeli ya *a- wa* kwa usahihi.<br>• Atunge sentensi kwa kutumia msamiati unaohusiana na ngeli ya *a- wa* | **Sarufi**<br>a) **Ngeli ya *A-Wa* (watu wa shuleni)**<br>Mwalimu **a**nafundisha – Walimu **wa**nafundisha<br>Mwanafunzi **a**nasoma– Wanafunzi **wa**nasoma<br>Msichana **a**nacheza– Wasichana **wa**nacheza | • Kutambua na kutaja nomino zinazotokana na ngeli ya *a-wa* katika umoja na wingi<br>• Kutunga sentensi kwa umoja na wingi kwa kuonyesha upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya *a-wa* |
| • Ataje vivumishi vya sifa<br>• Atumie vivumishi vya sifa katika sentensi | b) Vivumishi vya sifa:<br>• Mwalimu **mzuri**<br>• Walimu **wazuri**<br>• Msichana **mrembo**<br>• Wasichana **warembo**<br>• Mwanafunzi **mfupi** Wanafunzi **wafupi**<br>**Kuandika (Dialojia)**<br>Sentensi zenye kauli za maamkuzi na maneno ya adabu k.v.<br>- **Kato**: Nyumbani ni kwema?<br>- **Atim**: Ndiyo! Ni kwema kabisa ... | • Kutaja vivumishi vya sifa<br>• Kutunga sentensi fupi ukitumia vivumishi vya sifa |

| Umilisi | Yaliyomo | Shughuli zinazopendekezwa |
|---|---|---|
| • Aandike sentensi za dialojia zenye kauli za salamu na maneno ya adabu | **Kuandika (Dialojia)**<br>Sentensi zenye kauli za maamkuzi na maneno ya adabu k.v.<br>- **Kato**: Nyumbani ni kwema?<br>- **Atim**: Ndiyo! Ni kwema kabisa ... | • Kuandika sentensi za dialojia zisizopungua majibizano manne zenye kauli za salamu na adabu |

**Tathmini:**

i) Kusalimia na kujibu salamu
ii) Kutunga sentensi
iii) Kubainisha matumizi ya salamu na msamiati wa maneno ya adabu
iv) Kusoma sauti za Kiswahili vizuri
v) Kujaza mapengo
vi) Kudhihirisha
vii) Kuigiza
viii) Kutumia kamera au simu kunasa maigizo
ix) Uchunguzi k.v. usomaji, uigizaji, udhihirishaji/uonyeshaji

## MADA KUU 2: UKOO

**Usuli:** Mafunzo yatamwezesha mwanafunzi kutumia msamiati unaohusiana na ukoo na matumizi ya lugha yatakayomfaa katika kuwasiliana na watu wengine katika shughuli zake za kila siku.

**Matarajio:**

1. Mwanafunzi atambue msamiati unaohusiana na ukoo.
2. Atunge sentensi akitumia msamiati unaohusiana na ukoo pamoja na vipengele vya kisarufi katika mada husika.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Mawasiliano:
  - kusikiliza kwa makini
  - kutamka kwa usahihi
  - kusoma kwa ufasaha
  - kuandika kwa usahihi
  - kuwataja watu kwa hadhi na heshima zao

- Upendo:
  - kujulia jamaa hali
  - kuwajali wengine
  - kuongea kwa adabu

- Kushirikiana kwa:
  - Kutumia matamshi na vitendo vinavyoendeleza upendo na ushirikiano
  - kutii na kuheshimu watu wa ukoo.

- Kujitambua:
  - kuelezea asili yake
  - kutambua jukumu lake katika jamii.

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| **Mwanafunzi:**<br>• Asimulie hadithi fupi kuhusu ukoo | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>(a) Hadithi fupi kuhusu ukoo | • Kutaja majina ya ukoo<br>• Kuelezea majina ya ukoo<br>• Kusimulia hadithi kuhusu ukoo<br>• Kusoma kwa sauti |
| • Atambue msamiati wa ukoo.<br>• Atamke msamiati wa ukoo kwa usahihi | **(a) Msamiati**<br>Mjomba, babu, nyanya, ami, shangazi, mpwa, binamu, baba mdogo, | • Kutamka msamiati unaohusu ukoo<br>• Kutaja msamiati wa ukoo. |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| | mama mdogo, mjukuu, baba wa kambo, mama wa kambo | • Kufanya utafiti kuhusu ukoo wake na kuwasilisha mkururo wa familia yake. |
| • Asome hadithi kuhusu haki za watoto | **Kusoma**<br>Hadithi fupi kuhusu haki za watoto | • kusoma hadithi kuhusu haki za mtoto<br>• kutaja haki za mtoto zinazojitokeza katika makala |
| • Atambue njeo ya wakati uliopo<br>• Atunge sentensi katika wakati uliopo | **Sarufi**<br>a) Njeo: - na-<br>- Mjomba a**na**kula.<br>- Wajomba wa**na**kula.<br>- Mwalimu a**na**kula<br>- Walimu wa**na**kula<br>- Mwanafunzi a**na**soma<br>- Wanafunzi wa**na**soma<br>-Mlinzi anakimbia<br>-Walinzi wa**na**kimbia | • Kutunga sentensi kwa kutumia njeo ya –na- |
| • Atambue njeo ya wakati uliopita<br>• Atumie njeo ya wakati uliopita katika sentensi. | **a)** Njeo: ya – **Li-**<br>- Baba a**li**kuja<br>- Akinababa wa**li**kuja<br>- Mama a**li**pika<br>- Akinamama wa**li**pika | • Kutunga sentensi kwa kutumia njeo ya **-Li-** |
| Atunge sentensi kwa kutumia vionyesh | Ch) Vionyeshi<br>- huyu – hawa<br>- huyo – hao<br>- yule – wale | • Kutaja vionyeshi katika ngeli ya *a- wa*<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia vionyeshi |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Atunge sentensi kwa kutumia viunganishi | d) Viunganishi:<br>- na, lakini, au, ama, Mfano wa sentensi<br>- Mama na baba wanalima.<br>- Huyu ni mwalimu au mwanafunzi?<br>- Ninataka keki lakini sina pesa. | • Kutaja viunganishi husika<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia viunganishi kwa usahihi |
| Aandike hadithi kuhusu ukoo | **Kuandika**<br>Insha ya kuongozwa kuhusu ukoo | Kuandika insha ya kuongozwa |

**Tathmini:**

- Kutamka msamiati wa ukoo kwa usahihi
- Kueleza asili ya ukoo wake
- Kutunga sentensi kwa kutumia majina ya ukoo
- Kuandika maneno na sentensi kwa tahajia sahihi
- Kuandika insha ya mwongozo
- Kuandika msamiati wa ukoo na maelezo yake

## MADA KUU 3: MWILI WA BINADAMU

**Usuli:** Mafunzo haya yatamwezesha mwanafunzi kujitambua kwa kufahamu sehemu za mwili wake, kazi za sehemu hizo na namna ya kuzitunza. Katika mada hii mwanafunzi atatamka msamiati kwa usahihi na kuutumia katika miundo ya sentensi.

**Matarajio:** Mwanafunzi abainishe msamiati wa sehemu za mwili pamoja na vipengele vya kisarufi na kuvitumia katika mawasiliano.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Kuwasiliana:
  - matamshi bora
  - kusikiliza kwa makini
  - kuandika
  - kusoma kwa ufasaha
- Kujitambua:
  - kutaja sehemu za mwili wake na kazi zake
  - kuthamini sehemu zake za mwili
  - kutunza sehemu zake za mwili
- Kuwajibika:
  - kutambua sehemu za mwili wake
  - kutunza sehemu za mwili wake

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Mwanafunzi:<br>• Atambue sehemu za mwili wa binadamu kwa Kiswahili<br>• Afasiri mchoro wa sehemu za mwili wa binadam | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>(a) Hadithi kuhusu sehemu za mwili | • Kutaja sehemu za mwili wa binadamu<br>• Kuambatanisha jina na sehemu za mwili wa binadamu<br>• Kuonyesha sehemu za mwili kwa kuzigusa |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Atambue majina ya sehemu za mwili wa binadamu | **(a) Msamiati**<br>shavu, kidevu, kinywa, meno, ulimi, shingo, bega, kifua, ukwapa, mgongo, tumbo, kitovu, kiuno, paja, goti, wayo, kisigino, kidole, ukucha, kiganja, kiwiko | • Kutaja majina ya sehemu za mwili<br>• Kutamka msamiati wa sehemu za mwili<br>• Kuimba wimbo kuhusu sehemu za mwili wa binadamu<br>• Kutaja kazi za baadhi ya sehemu za mwili wa binadamu<br>• kuambatanisha sehemu za mwili wa binadamu na kazi zake |
| • Asome makala kuhusu kazi za mwili wa binadamu<br>• Atambue kazi za baadhi ya sehemu za mwili wa binadamu | **Kusoma**<br>Makala kuhusu kazi za baadhi ya sehemu za mwili wa binadamu | • Kutumia mtandao wa intaneti kupata mchoro wenye sehemu za nje za mwili wa binadamu.<br>• Kufasiri mchoro/picha ya sehemu za mwili<br>• kueleza kazi za sehemu za mwili wa binadamu |
| • Atambue nomino katika ngeli ya *U-I*<br>• Atumienomino za ngeli ya *u – i* katika kutunga sentensi | **Sarufi**<br>a) Ngeli ya *U-I* (***m-mi***)<br>mguu – miguu<br>mgongo – migongo<br>mkono – mikono<br>mdomo – midomo<br>mfano:<br>- Mguu **u**naniuma.<br>miguu **i**naniuma. | • Kutaja nomino katika ngeli ya *U-I* zinazohusiana na mwili wa binadamu<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli ya *U –I* kwa umoja na wingi. |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| | - Mkono **u**mechafuka.<br>- Mikono **i**mechafuka. | • Kusoma sentensi zinazohusiana na ngeli ya *U-I*. |
| • Atambue nomino katika ngeli ya ***li – ya***<br>• Atunge sentensi kutumia msamiati katika ngeli ya *li- ya*. | b) Ngeli ya Li-ya (*Ji-ma*)<br><br>- Jicho – macho<br>- Jino – meno<br>- Sikio – maskio<br>- Goti – magoti<br>mifano ya sentensi<br>- Jicho **li**naona<br>Macho **ya**naona<br>- Sikio **li**nasikia<br>Masikio **ya**nasikia | • Kutaja nomino katika ngeli ya: *Li- Ya* zinazohusiana na sehemu za mwili.<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli ya *Li- Ya* kwa umoja na wingi.<br>• kusoma sentensi zinazohusiana na ngeli ya *Li- Ya* |
| | Ch) Ngeli ya *Ki-Vi*<br>- Kidole – Vidole<br>- Kichwa – vichwa<br>- Kidevu – videvu<br><br>**Mifano ya sentensi**<br>- Kidole **ki**naandika<br>- Vidole **vi**naandika<br>- Kichwa **ki**na mvi<br>- Vichwa **vi**na mvi | • Kutaja majina katika ngeli ya Ki – Vi yanayohusiana na mwili wa binadamu.<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli ya *Ki – Vi* kwa umoja na wingi<br>• Kusoma sentensi zinazohusiana na ngeli ya *Ki- Vi*. |
| • Aandike insha kwa mpangilio unaofaa | **Kuandika**<br>Insha ya kuongozwa kuhusu namna ya kudumisha usafi wa sehemu za mwili. | • Kueleza namna ya kudumisha usafi wa sehemu za mwili |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| | | • Kujaza mapengo kwa kutumia maneno yanayofaa<br>Kuandika insha ya kuongozwa |

**Tathmini:**

- Kutamka sehemu za mwili vizuri.
- Kuambatanisha sehemu za mwili na msamiati wake
- Kutunga sentensi fupi
- Kutoa maelezo, k.v. Kazi za sehemu za mwili

## MADA KUU 4: HESABU

**Usuli:** Mafunzo haya yanalenga kumpa mwanafunzi maarifa na ujuzi wa kutambua msamiati wa hesabu na miundo ya lugha.
Yatamwezesha kuwasiliana katika mazingira ya masuala yahesabu.

**Matarajio:** Mwanafunzi aweze kuhesabu na kutambua alama zinazotumika katika hesabu.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Kuwasiliana kwa:
  - kutamka nambari kwa ufasaha
  - kusikiliza kwa makini
  - kuzungumza
  - kuandika
  - kusoma kwa ufasaha
- Kuainisha tarakimu
- Kuthamini

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| **Mwanafunzi:**<br>• Atamke tarakimu kwa maneno<br>• Ahesabu kutoka sifuri hadi mia moja | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>a) Kuhesabu 0 - 100<br>moja, mbili, tatu, nne, tano<br>mia mbili, mia tatu, mia nne, mia tano | • Kuhesabu tarakimu kutoka 0 hadi 100<br>• Kusoma tarakimu na maneno<br>• Kuambatanisha tarakimu na maneno |
| • Atege vitendawili<br>• Ategue vitendawili | b) Vitendawili vinavyohusiana na hesabu.<br>Mifano:<br>• Haba na haba hujaza kibaba. | • Kutambua vitendawili vinavyohusiana na hesabu.<br>• Kutega vitendawili<br>• Kutegua vitendawili<br>• Kufanya utafiti kuhusu vitendawili |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| | • Nina wasichana watatu, mmoja akitoka sili chakula. | vinavyojulikana katika jamii yake. |
| • Atambue alama za hesabu<br>• Atumie alama za hesabu katika sentensi | **Ch) Msamiati**<br>Alama za hesabu:<br>**Alama**<br>+ kuongeza<br>- kuondoa<br>x kuzidisha<br>÷ kugawa<br>= kusawazisha | • Kutaja alama za hesabu<br>• Kueleza kuhusu alama za hesabu<br>• Kutumia alama za hesabu kwenye kikokotoo kupata matokeo mapya.<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia alama za hesabu |
| • Asome kuhusu saa<br>• Aelezee saa | **Kusoma**<br>Kusoma saa | • Kusoma saa<br>• Kueleza saa |
| • Atambue na kutunga sentensi kwa kutumia kiulizi *ngapi?* | **sarufi**<br>**(a)** Kiulizi: *ngapi?*<br>Mfano:<br>- Sasa ni saa ngapi?<br>- Umepata alama ngapi?<br>- Wiki ina siku ngapi?<br>- Siku ina saa ngapi?<br>- Mwaka una miezi mingapi? | • Kueleza kuhusu matumizi ya kiulizi *ngapi?*<br>• Kutambua matumizi ya kiulizi *ngapi?*<br>• Kutunga sentensi kuonyesha matumizi ya kiulizi *ngapi?* |
| • Ataje vivumishi vya idadi kamili<br>• Atunge sentensi kwa kutumia vivumishi vya | b) Vivumishi vya idadi (miezi ya mwaka)<br>- Mwezi mmoja<br>- Miezi miwili | • Kutaja vivumishi vya idadi kamili<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia vivumishi vya |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| idadi kamili kwa miezi ya mwaka.<br>• Atambue miezi ya mwaka | - Miezi saba | idadi kamili kwa kutumia miezi katika mwaka<br>Kutaja miezi katika mwaka |
| Akamilishe insha kuhusu siku za wiki. | **Kuandika**<br>Insha ya kuongozwa kuhusu siku za wiki. | Kutaja siku za wiki<br>Kujaza mapengo katika insha ya kuongozwa kuhusu siku za wiki |

**Tathmini:**

- Kuchunguza k.v. matamshi, usomaji, n.k.
- Kubadilisha tarakimu kwa maneno
- Kutunga sentensi kwa kutumia kiulizi ngapi?
- Kuambatanisha alama za hesabu na maneno
- Kuandika nambari za hesabu kwa usahihi.

# MUHULA WA PILI

## MADA KUU 1: MAVAZI NA RANGI

**Usuli:** Mafunzo haya yatamwezesha mwanafunzi kufahamu msamiati wa mavazi na rangi pamoja na miundo ya lugha itakayohusishwa katika mawasiliano yake.

**Matarajio:** Mwanafunzi atambue na kubainisha msamiati wa rangi, mavazi, sarufi pamoja na matumizi yake.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Kuwasiliana vyema:
  - matamshi sahihi
  - kusikiliza kwa makini
  - kusoma kwa ufasaha
  - kuzungumza kwa ufasaha
- Kutambua:
  - kubainisha rangi mbalimbali
  - kubainisha mavazi mbalimbali
  - kuhusisha rangi na vitu katika mazingira yake
  - kupambanua mavazi kulingana na jinsi na umri
- Kuthamini kazi za sanaa:
  - kuthamini jinsi rangi mbalimbali zilivyotumika
  - kuthamini mitindo ya mavazi mbalimbali
- Kuwajibika na kujali:
  - kutunza mavazi
  - kuvaa kwa heshima
  - kupambanua mavazi kijinsi na kiumri

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Mwanafunzi:<br>Ataje rangi na maana za bendera ya taifa la Uganda | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>(a) Mjadala kuhusu rangi za bendera ya taifa na maana ya rangi hizo | • Kutamka maneno kwa usahihi<br>• Kufasiri rangi za bendera<br>• Kueleza maana za rangi za bendera ya taifa |
| Atamke msamiati wa rangi na mavazi.<br>Atumie msamiati wa rangi na mavazi katika sentensi. | **(a) Msamiati**<br>Rangi: -eupe, eusi, -ekundu, manjano, bluu, -kijivu, zambarau, kijani, kahawia, rangi ya chungwa, waridi | • Kutambua rangi mbalimbali<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia rangi mbalimbali |
| Asome hadithi fupi kuhusu majina ya mavazi | **Kusoma**<br>Aina za mavazi: suruali, shati, rinda, sketi, blauzi, koti, chepeo, viatu, kaptula, mshipi, kofia | • Kutaja aina za mavazi<br>• Kueleza jinsi mavazi yanavyovaliwa kijinsia.<br>• Kufanya utafiti maktabani au kwenye mtandao wa intaneti kuhusu mavazi maalumu kulingana na hali mbalimbali. |
| • Atambue nomino katika ngeli za *I – Zi*, U-I na *Ki – Vi* zinazohusiana na mavazi.<br><br>• Atunge sentensi katika umoja na wingi kwa kutumia msamiati wa ngeli za *I-Zi* na *KI- Vi* | **Sarufi**<br>a) Ngeli:<br>i) *I- Zi-*<br>Nguo **i**nang'aa.<br>Nguo **zi**nang'aa.<br>ii) *U-I-*<br>Mshipi **u**mekatika<br>Mishipi **i**mekatika<br>*iii) Ki- Vi*<br>Kiatu **ki**meharibika.<br>Viatu **vi**meharibika. | • Kutaja nomino katika ngeli za *I-Zi*, *U-I*, *Ki-Vi*<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli husika |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| • Atambue vivumishi vinavyohusiana na mavazi na rangi<br>• Atumie vivumishi katika sentensi | a) Vivumishi vya sifa. Mfano:<br>-suruali nyekund<br>- kiatu cheusi<br>- viatu vyeusi | • Kutaja vivumishi vya sifa<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia vivumishi vya sifa |
| • Atambue vitenzi vinavyohusiana na rangi na mavazi<br>• Atumie vitenzi katika sentensi | Ch) Vitenzi vinavyohusiana na mavazi: vua, fua, funika, piga pasi, osha | • Kutaja vitenzi vinavyohusiana na mavazi na rangi |
| • Atambue vinyume vya vitenzi<br>• Aambatanishe vitenzi na vinyume vyake | (d) Kinyume:<br>- vaa – vua<br>- anika – anua<br>- eusi – eupe | • Kutambua vitenzi<br>• Kuandika vinyume vya vitenzi<br>• Kuambatanisha vitenzi na vinyume vyake |
| • Aandike rangi za upinde wa mvua | **Kuandika (Kuchora)**<br>Rangi za upinde wa mvua | • Kuchora na kutaja rangi za upinde wa mvua. |

**Tathmini:**

- Kuchunguza:
  - matamshi na usomaji
  - mazungumzo
  - usikilizaji
- Kuambatanisha msamiati wa rangi za mavazi na michoro
- Kutunga sentensi sahihi
- Kubainisha rangi na mavazi mbalimbali
- Kupambanua mavazi ya kike, kiume, vijana, wazee na watoto
- Kuandika insha ya mwongozo kuhusu rangi na mavazi

## MADA KUU 2: WANYAMA

**Usuli:** Mafunzo haya yatamwezesha mwanafunzi kukuza maarifa yake kuhusu wanyama kwa kuzingatia msamiati na vipengele vya ngeli, nyakati, vitenzi na vihusishi ili kuimarisha mawasiliano yake.

**Matarajio:**

1. Mwanafunzi atambue msamiati unaohusiana na wanyama na watoto wao.
2. Atunge sentensi akitumia miundo ya lugha iliyopendekezwa katika mada hii.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Kuwasiliana kikamilifu:
  - kutamka maneno
  - kusikiliza kwa makini
  - kusoma kwa ufasaha
  - kuandika kwa tahajia sahihi
- Kuwajibika:
  - kuthamini wanyama
- Kupenda:
  - kutunza wanyama vizuri

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Mwanafunzi:<br>• Atambue tashbihi za wanyama<br>• Atumie tashbihi katika mazungumzo | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>a) Tashbihi zinazohusiana na wanyama:<br>Mfano:<br>- mrefu kama twiga<br>- mwepesi kama swara<br>- mkali kama simba | • Kutamka manenokwa usahihi.<br>• Kutaja tashbihi zinazohusiana na wanyama<br>• Kueleza maana ya tashbihi |
| • Atambue wanyama na watoto wao. | **b) Msamiati**<br>Wanyama wa nyumbani na watoto wao kama vile: | • Kutaja majina ya watoto wa wanyama<br>• Kutumia msamiati unaohusiana na |

<table>
<tr><th>UMILISI</th><th>YALIYOMO</th><th>SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA</th></tr>
<tr>
<td>• Atumie msamiati katika sentensi</td>
<td><table>
<tr><th>Mzazi</th><th>Mtoto</th></tr>
<tr><td>Ng'ombe</td><td>Ndama</td></tr>
<tr><td>Kuku</td><td>Kifaranga</td></tr>
<tr><td>Kondoo</td><td>Mwanakondoo</td></tr>
</table></td>
<td>wanyama pamoja na watoto wao kutunga sentensi</td>
</tr>
<tr>
<td>Asome taarifa kuhusu namna wanyama wanavyotunza watoto wao</td>
<td>Kusoma<br>Taarifa fupi kuhusu namna wanyama wanavyotunza watoto wao</td>
<td>Kutaja namna wanyama wanavyotunza watoto wao</td>
</tr>
<tr>
<td>• Atambue nomino katika ngeli ya A-Wa<br>• Atumie nomino za ngeli katika sentensi kwa umoja na wingi</td>
<td>Sarufi<br>a) Ngeli ya A- Wa-:<br>- Ng'ombe amepotea.<br>- Ng'ombe wamepotea.<br>- Kifaranga anatetemeka.<br>- Vifaranga wanatetemeka.</td>
<td>• Kufanya kazi-mradi kuhusu jinsi wanyama wanavyofaa kutunzwa katika mazingira yao.<br>• Kutambua nomino katika ngeli ya A- Wa-<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia nomino katika ngeli ya a- wa kwa umoja na wingi</td>
</tr>
<tr>
<td>• Atambue viwakilishi vya wakati ujao<br>• Atunge sentensi katika wakati ujao</td>
<td>(b) Njeo ya –ta-<br>Mfano:<br>- Kuku a<u>t</u>ataga<br>- Ng'ombe atakamwa<br>- Mbuzi atazaa</td>
<td>• Kutambua kiambishi cha wakati ujao<br>• Kutunga sentensi katika wakati ujao kutumia nomino za ngeli ya a- wa</td>
</tr>
<tr>
<td>Atambue matumizi ya vihusishi 'katika' na 'ni'<br>Atumie 'katika' na 'ni' katika sentensi</td>
<td>Ch) Matumizi ya 'katika' na '-ni'.<br>Mfano:<br>Ng'ombe yuko zizini.<br>Ng'ombe wako katika zizi.</td>
<td>• Kueleza matumizi ya 'katika' na '-ni'<br>• Kutunga sentensi kuonyesha matumizi ya 'katika' na 'ni'</td>
</tr>
</table>

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Aandike insha ya mwongozo kuhusu "Mnyama nimpendaye" | **Kuandika**<br>Insha ya kuongozwa kuhusu *"Mnyama nimpendaye"* | • Kuandika insha kuhusu "**Mnyama nimpendaye"** |

**Tathmini:**

- Kuchunguza:
  - matamshi
  - kusikiliza
  - kusoma
- Kutaja:
  - majina ya wanyama
  - watoto wa wanyama
- Kuchora na kutaja k.v.: mnyama na mtoto wake
- Kukamilisha tashbihi k.v. imara kama __ (simba).
- Kutunga sentensi sahihi
- Kujaza mapengo

## MADA KUU 3: AFYA NA USAFI

**Usuli:** Mafunzo haya yanalenga kuongeza maarifa na ujuzi wa mwanafunzi kuhusiana na msamiati wa afya, usafi, wadudu waletao magonjwa na magonjwa yenyewe kwa kutumia miundo ya lugha iliyopendekezwa ili kuimarisha uwezo wake wa kuwasiliana katika Kiswahili.

**Matarajio:** Mwanafunzi awe na ufahamu wa kimsingi kuhusu afya na usafi na autumie msamiati huo pamoja na miundo ya lugha katika mawasiliano.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Kuwasiliana:
  - kutamka kwa ufasaha
  - kusikiliza kwa makini
  - kuandika
  - kusoma kwa ufasaha
- Kutambua:
  - wadudu na maradhi wanayosababisha
  - Kuwajibika:
  - kujikinga dhidi ya magonjwa na vyanzo vyake
- Kujali:
  - kuweka mazingira safi

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Mwanafunzi:<br>• Asikilize kwa makini hadithi kuhusu wadudu wanaoeneza magonjwa<br>• Asimulie hadithi ya kuongozwa kuhusu wadudu wanaoeneza magonjwa<br>• Atambue wadudu wanaoeneza magonjwa | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>a) Hadithi kuhusu wadudu wanaoeneza, magonjwa au maradhi kama: mbu, nzi, mbung'o, viroboto, funza, | • Kufasiri picha na michoro ya wadudu wanaosababisha magonjwa.<br>• Kusimulia hadithi kuhusiana na wadudu na magonjwa<br>• Kutaja aina za magonjwa mbalimbali |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| | | • Kutoa maelezo kuhusu wadudu wanaoeneza magonjwa |
| • Atamke msamiati wa magonjwa<br>• Atumie msamiati wa magonjwa katika sentensi<br>• Atunge sentensi kwa kutumia msamiati wa magonjwa. | **a) Msamiati**<br>Magonjwa kama: kipindupindu, malaria, malale, funza | • Kutunga sentensi kwa kutumia msamiati unaohusiana na magonjwa<br>• Kuambatanisha;<br>• -mdudu na picha/mchoro wake<br>-mdudu na ugonjwa anaosababisha |
| • Asome makala kuhusu kinga dhidi ya magonjwa<br>• Atambue kinga dhidi ya magonjwa | **Kusoma**<br>Makala kuhusu kinga dhidi ya magonjwa | • Kusoma makala kuhusu kinga dhidi ya magonjwa<br>• Kutaja kinga dhidi ya magonjwa<br>• Kueleza ujumbe wa taarifa kutokana na makala. |
| • Atambuenomino katika ngeli za *U – Ya* na *ya - ya*<br>• Atumie nomino za ngeli husika katika kutunga sentensi kwa umoja na wingi | **Sarufi**<br>a) Ngeli:<br>i) *U- Ya*- Mfano:<br>-Ugonjwa **u**meenea.<br>-Magonjwa **ya**meenea.<br>i) *–Ya –Ya* Mfano:<br>Maji **ya**mechemshwa | • Kutaja nomino katika ngeliya u- ya, ya - ya<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia nomino katika ngeli za u- ya na ya- ya |
| • Atambue vitenzi vinavyohusiana na magonjwa<br>• Atumie vitenzi katika kutunga sentensi | b) Vitenzi vinavyohusiana na magonjwa:<br>Tibu, kinga, dunga meza tapika<br>Mfano:<br>-Daktari amemdunga sindano. | • Kutaja vitenzi vinavyohusiana na magonjwa na wadudu<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia vitenzi husika |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| | -Daktari amewadunga sindano. | |
| • Atambue viwakilishi vya nafsi<br>• Atunge sentensi kwa kutumia viwakilishi vya nafsi katika umoja na wingi | ch) Nafsi<br>**Umoja** **Wingi**<br>Mimi Sisi<br>Wewe Nyinyi<br>Yeye Wao<br>Kwa mfano:<br>Mimi nimeugua malaria.<br>Sisi tumeugua malaria. | • Kutaja viwakilishi vya nafsi katika umoja na wingi<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia viwakilishi vya nafsi katika umoja na wingi |
| Aandike insha ya mwongozo kuhusu mdudu hatari anayesababisha ugonjwa. | **Kuandika**<br>Insha ya kuongozwa kuhusu mdudu hatari anayesababisha ugonjwa | • Kueleza kuhusu mdudu hatari<br>• Kujaza mapengo katika insha ya mwongozo kuhusu mdudu hatari. |

**Tathmini**

- Kuchunguza k.v. kutamka, kusikiliza, kusoma
- Kutoa maelezo k.v. mdudu anayesababisha ugonjwa
- Kutunga sentensi
- Kukamilisha sentensi

## MADA KUU 4: SEHEMU ZA NYUMBANI

**Usuli:** Mafunzo haya yatamwezesha mwanafunzi kukuza ujuzi wake kuhusu msamiati wa sehemu za nyumbani. Kupitia mada hii, mwanafunzi ataweza kujifunza vipengele vya lugha vitakavyomwezesha kuzungumza lugha ya Kiswahili.

**Matarajio**: Mwanafunzi aweze kutambua msamiati wa sehemu za nyumbani na vitu vinavyopatikana katika sehemu hizo pamoja na kutumia vipengele vya sarufi katika mawasiliano.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Kuwasiliana kwa:
  - Matamshi bora
  - kusikiliza
  - kuandika
  - kusoma
- Kujali:
  - vyombo vya jikoni na sehemu za nyumbani
  - kutunza na kuthamini vitu vinavyopatikana nyumbani
- Kuwajibika kwa kutunza vyombo vya nyumbani

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| **Mwanafunzi;**<br>Asimulie hadithi ya kuongozwa kuhusu sehemu na vitu vinavyopatikana nyumbani. | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>(a) Hadithi ya kuongozwa kuhusu sehemu na vitu vya nyumbani. | Kusimulia hadithi ya kuongozwa kuhusu sehemu na vitu vya nyumbani. |
| • Atambue msamiati wa vitu vinavyopatikana nyumbani.<br>• Atumie msamiati wa sehemu na vitu vya | (a) **Msamiati:**<br>meko, vikombe, sahani, vijiko, sufuria, rafu, zizi, ua, baraza, kiunga, choo, | • Kutambua msamiati wa vitu vya nyumbani.<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia msamiati husika |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| nyumbani katika kutunga sentensi | ghala, makonge, mkeka, kamba,shona, suka | |
| • Asome kifungu cha maneno kuhusu sehemu za nyumbani | **Kusoma**<br>Kusoma kifungu cha maneno kuhusu sehemu za nyumbani | • Kusoma kwa sauti na kwa makini<br>• Kutaja sehemu za nyumbani<br>• Kueleza ujumbe wa hadithi |
| • Atambue nomino katika ngeli ya I- Zi, U- Zi<br>• Atumie nomino husika katika kutunga sentensi | **Sarufi**<br>**a) Ngeli:**<br>i) *i- zi-*:<br>Sahani **i**mepotea.<br>Sahani **zi**mepotea.<br>ii) *U- Zi*<br>Ukuta **u**mepambwa Kuta **zi**mepambwa | • Kutaja nomino katika ngeli *za I-Zi* na *U- Zi*<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia majina yangeli za i-zi na u- zi |
| • Atambue vivumishi vya sifa<br>• Atumie vivumishi vya sifa kutunga sentensi | b) Vivumishi vya sifa:<br>- Chumba kipana<br>Vyumba vipana<br>- Sahani safi | • Kubainisha vivumishi vya sifa na vya kumiliki<br>• Kutumia vivumishi vya sifa katika kutunga sentensi |
| - Atambue vimilikishi<br>- Atumie vivumishi vimilikishi kutunga sentensi. | Ch) Vivumishi vimilikishi:<br>- kijiko chetu<br>- vijiko vyetu | • Kutaja vivumishi vimilikishi<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia vivumishi vimilikishi katika umoja na wingi |
| Aandike sentensi kuhusu sehemu za nyumbani. | **Kuandika** | • Kuandika insha kwa tahajia sahihi<br>• Kutazama na kufasiri picha na michoro ya |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| | Kuandika insha inayohusu sehemu za nyumbani. | sehemu na vitu vya nyumbani. |

**Tathmini:**

- Kutunga sentensi.
- Kukamilisha sentensi.
- Kupanga au kuunganisha sentensi kuandika insha.
- Kuambatanisha chombo na msamiati wake.
- Kuchora sehemu za nyumbani na vyombo vya jikoni.

# MUHULA WA TATU

## MADA KUU1: MICHEZO

**Usuli:** Mafunzo haya yanalenga kumpa mwanafunzi ufahamu na utambuzi wa michezo na manufaa yake. Msamiati wa michezo, vifaa vya michezo na vipengele vya lugha atakavyojifunza vitamwezesha mwanafunzi kuchangia mawasiliano katika muktadha wa michezo.

**Matarajio**: Mwanafunzi awe na ufahamu wa kimsingi wa msamiati wa michezo, vifaa vya michezo na kutumia vipengele vya lugha vilivyoteuliwa katika kuwasiliana.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Kuwasiliana:
  - kusikiliza kwa makini
  - kutamka maneno kwa ufasaha
  - kuandika kwa tahajia sahihi
- Kutambua:
  - michezo, vifaa vya michezo, umuhimu wa michezo
- Kuwajibika:
  - kwa kutii sheria na kanuni za michezo
- Kushirikiana:
  - kutii sheria na kanuni za michezo.

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Mwanafunzi:<br>• Afasiri picha kuhusu michezo.<br>• Asimulie hadithi ya kuongozwa kuhusu picha za michezo | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>a) Hadithi ya picha kuhusu michezo | • Kutaja vifaa vya michezo<br>• Kufasiri picha /michoro kuhusu michezo.<br>• Kutafuta michezo yoyote mtandaoni na kutambua wachezaji hodari katika michezo hiyo. |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| • Atambue msamiati wa michezo<br>• Atumie msamiati wa michezo katika sentensi | a) **Msamiati:**<br>kandanda, riadha, mpira wa pete, mpira wa vikapu, voliboli, ndondi, n.k. | • Kutaja msamiati wa michezo mbalimbali<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia msamiati wa michezo |
| Asome hadithi kuhusu umuhimu wa michezo | **Kusoma**<br>Hadithi kuhusu umuhimu wa michezo | • Kusoma kwa sauti<br>• Kueleza kuhusu umuhimu wa michezo. |
| • Atambue nomino katika ngeli ya *U-I*<br>• Atumie nomino za ngeli ya *U-I* katika kutunga sentensi kwa umoja na wingi<br>• Atambue viashiria katika ngeli ya *U-I* | **Sarufi**<br>a) Ngeliya *U-I-*<br>- Michezo **u**livutia.<br>- Michezo **i**livutia. | • Kutaja nomino katika ngeli ya *U-I* zinazohusiana na michezo.<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia nomino katika ngeli ya u-i, |
| Atunge sentensi kwa kutumia vionyeshi katika umoja na wingi | b) Vionyeshi:<br>- mpira **huu** – mipira **hii**<br>- mpira **huo** – mpira **hiyo**<br>- mpira **ule** – mipira **ile** | • Kutaja vionyeshi katika ngeli ya u-i<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia vionyeshi. |
| • Atambue matumizi ya **'kwa'**<br>• Atumie'**kwa'**katika kutunga sentensi | Ch) Matumizi ya "kwa":<br>Mfano:<br>- Alifunga bao **kwa** kichwa.<br>- Alitoa pasi **kwa** mwenzake | • Kutambua matumizi ya 'kwa'<br>• Kutunga sentensi zenye **'kwa'** |
| • Atambue matumizi ya viulizi *–pi?* na *gani?* | c) Viulizi: | • Kutambua viulizi **–pi?** na **gani?** |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| • Atunge sentensi kwa kuonyesha matumizi ya viulizi *–pi?* na *gani?* | -pi?<br>-gani? Mfano:<br>-Mchezaji yu**pi** ni nyota?<br>-Ni timu **gani** ilishinda? | • Kutunga sentesi kwa kutumia viulizi husika.<br>• Kueleza kuhusu matumizi ya viulizi **–pi?** na **gani?** |
| Aandike insha ya kuongozwa kuhusu picha za michezo | **Kuandika**<br>Kuandika insha ya kuongozwa kuhusu picha za mchezo | • Kuandika kwa kuzingatia tahajia sahihi<br>• Kuambatanisha michezo na vifaa vyake.<br>• Kuandika insha kwa kurejelea picha |

**Tathmini:**

- Kuchunguza:
  - matamshi, kusoma, kusikiliza
- Kukamilisha sentensi kwa kujaza mapengo
- Kutunga sentensi
- Kuchora na kutaja vifaa vya michezo
- Kufasiri picha/michoro
- Kuambatanisha vifaa vya michezo na michezo yenyewe

## MADA KUU 2: BIASHARA

**Usuli:** Mafunzo haya yatampa mwanafunzi fursa ya kuimarisha lugha inayotumika katika mazingira ya ununuzi na uuzaji. Mwanafunzi ashirikishwe katika shughuli zitakazomwezesha kujenga uzoefu wa kimawasiliano katika nyanja za uuzaji na ununuzi.

**Matarajio**: Mwanafunzi atumie msamiati wa shughuli za uuzaji na ununuzi pamoja na miundo ya lugha aliyojifunza kuwasiliana katika mazingira ya uuzaji na ununuzi.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Kuwasiliana kikamilifu:
  - kwa kuzungumza
  - kwa kusoma
  - kwa kuandika
- Mapatano kibiashara kwa:
  - matumizi ya lugha ya kushawishi na adabu
  - kutolaghai
- Kushirikiana kwa:
  - kutii kununi za kibiashara
  - kuzingatia sheria za kibiashara
- Kutoa uamuzi kwa kununua au kutonunua

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Mwanafunzi:<br>• Aigize kuhusu ununuzi na uuzaji dukani | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>a) Maigizo kuhusu ununuzi na uuzaji dukani | • Kutamka maneno kwa usahihi katika maigizo.<br>Kuigiza kuhusu ununuzi na uuzaji dukani<br>• Kutumia chombo cha kielektroniki kunasa video kuhusu shughuli za ununuzi na uuzaji. |

| | | |
|---|---|---|
| • Atambue msamiati unaohusiana na ununuzi na uuzaji dukani<br>• Atambue msamiati wa bidhaa za dukani. | a) **Msamiati**<br>Bidhaa zinazouzwa dukani k.v.:<br>sukari, sabuni, chumvi, kiberiti, unga, majani chai, maziwa, vitabu, n.k. | • Kutaja msamiati wa bidhaa dukani<br>• Kufasiri picha na michoro ya bidhaa.<br>• Kuambatanisha msamiati na bidhaa halisi. |
| • Asome taarifa kuhusu shughuli za sokoni<br>• Atambue shughuli za sokoni katika taarifa | **Kusoma**<br>Taarifa kuhusu shughuli za sokoni | • Kusoma kwa sauti<br>• Kutaja shughuli za sokoni |
| • Atambue nomino katika ngeli ya i-i<br>• Atumie nomino katika kutunga sentensi kwa umoja na wingi | **Sarufi ;** Ngeli ya *I-*<br>Mifano:<br>-Sukari **i**mepimwa.<br>-Chumvi **i**mekwisha. | • Kutaja nomino katika ngeli ya I-I zinazohusiana na bidhaa.<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia majina katika ngeli ya I- |
| Aandike insha ya mwongozo kuhusu shughuli za sokoni | **Kuandika**<br>Insha kuhusu shughuli za sokoni | • Kutaja shughuli za sokoni<br>• Kuandika insha kwa tahajia sahihi |

**Tathmini:**

- Kuchunguza k.v. kutamka maneno, kusikiliza matamshi, kuzungumza, uigizaji
- Kuambatanisha:
  - msamiati na picha/michoro
  - msamiati na bidhaa halisi
- Kukamilisha sentensi
- Kuandika
- Kutunga sentensi kudhihirisha

## MADA KUU 3: UONGOZI

**Usuli:** Mafunzo haya yatamwezesha mwanafunzi kuimarisha msamiati na miundo ya lugha inayohusiana na uongozi pamoja na majukumu shuleni. Haya yatampa mwanafunzi uzoefu wa kujieleza akitumia lugha ya Kiswahili katika mazingira mbalimbali ya uongozi na kukuza uwezo wake wa kuwasiliana.

**Matarajio**: Mwanafunzi awe na uwezo wa kutumia msamiati unaohusiana na uongozi pamoja na majukumu shuleni katika mawasiliano huku akitumia vipengele vya kisarufi vilivyoteuliwa katika mada hii.

**Stadi za kimaisha na maadili**

- Kuwasiliana:
  - kimatamshi
  - kwa kusoma kiufasaha
- Kushirikiana:
  - kuheshimu uongozi
  - kutii sheria na kanuni
  - katika kuchagua viongozi
- Kujiamini na kujithamini
- Kuwa na msimamo thabiti
  - kuwa na uwazi
  - kuheshimu mawazo ya wengine
  - kujitolea
  - kutetea haki zako na za wengine
  - kushawishi wengine kwa wema
  - kutetea maamuzi ya haki

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| Mwanafunzi:<br>• Ataje majukumu ya uongozi | **Kusikiliza na kuzungumza**<br>a) Mjadala kuhusu majukumu ya uongozi | • Kutaja majukumu ya viongozi.<br>• Kuimba wimbo kuhusu viongozi<br>• Kueleza majukumu ya:mwalimu mkuu na kiranja |
| • Atambue msamiati wa viongozi shuleni<br>• Atumie msamiati wa uongozi katika kutunga sentensi | b) Msamiati<br>mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu, mwalimu, mwalimu wa darasa, mwalimu wa zamu, kiranja wa darasa, kiranja wa michezo, mdhibiti wakati, kiranja wa burudani | • Kutaja msamiati wa viongozi shuleni |
| • Asome taarifa kuhusu majukumu ya mwalimu mkuu<br>• Atambue majukumu ya mwalimu mkuu | **Kusoma**<br>Taarifa kuhusu majukumu ya mwalimu mkuu | Kusoma kwa sauti |
| • Atambue nomino katika ngeli ya *a-wa*<br>• Atumie nomino katika ngeli ya *a-wa* kutunga sentensi | **Sarufi**<br>a) Ngeli ya *A- Wa-*<br>Mfano:<br>Kiranja **a**lituhutubia.<br>Viranja **wa**lituhutubia. | • Kutaja nomino za ngeli ya a-wa<br>• Kutunga sentensi kwa kuonyesha matumizi ya nomino za *a-wa* katika umoja na wingi. |
| • Atambue ukanushaji wa nafsi.<br>• Akanushe sentensi kwa kuzingatia nafsi | b) Ukanushaji wa nafsi k.v:<br>- Ni – si<br>- U – hu<br>- A – ha<br>- Tu – hatu nk. | • Kutambua vikanushi vya nafsi kwa umoja na wingi<br>• Kukanusha sentensi kwa kuzingatia nafsi husika |

| UMILISI | YALIYOMO | SHUGHULI ZINAZOPENDEKEZWA |
|---|---|---|
| | | |
| Atambue shughuli za shuleni | Ch) Vitenzi kuhusu shughuli za shuleni: kuandika, kusoma kufagia, kuimba, kufundisha, kucheza, kuongoza, kuadhibu | • Kutaja shughuli za shuleni.<br>• Kutunga sentensi kwa kutumia shughuli za shuleni |
| Aandike insha kwa kupanga sentensi kuhusu kiranja yeyote. | **Kuandika**<br>Insha ya kuongozwa kwa kupanga kwa mfulilizo sentensi kuhusu kiranja yeyote. | Kuandika insha |

**Tathmini:**

- Kuchunguza k.v.
  - matamshi
  - kusikiliza
  - kuzungumza
  - kudhihirisha
  - kusoma
  - kuimba
- Kukamilisha sentensi
- Kutunga sentensi
- Kukanusha
- Kuandika
- Kuambatanisha viongozi na majukumu yao.
- Baadaya ya somo hili wanafunzi wanaweza kufundishwa uongozi nje ya shule kama kwenye serikali.

NCDC
NATIONAL CURRICULUM DEVELOPMENT CENTRE

National Curriculum Development Centre
P.O. Box 7002, Kampala.
www.ncdc.go.ug

ISBN 978-9970-675-56-2